WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

TAASISI YA ELIMU TANZANIA

MUHTASARI WA SOMO LA LUGHA YA ALAMA YA TANZANIA (LAT)

KWA MWALIMU TARAJALI WA FANI YA UZIWI

ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2019

Toleo la Kwanza 2019

ISBN: 978-9976-61-834-1

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam
Tanzania

Simu: +255 222 773 005
Faksi: +255 222 774 420
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). Muhtasari wa Somo la Lugha ya Alama ya Tanzania kwa Mwalimu Tarajali Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu. Dar es Salaam: Taasisi ya ELimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kuutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

Idhini

Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kumuandaa mwalimu tarajali kuwa mahiri na mwenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati na kwa weledi. Mwalimu huyo atafundisha katika shule za msingi zinazodahili wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Mwalimu tarajali atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhitimu mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu na kufaulu mafunzo ya nadharia na mafunzo ya ualimu kwa vitendo.

Muhtasari huu umeidhinishwa kuwa ni wa somo la Lugha ya Alama ya Tanzania katika Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kaimu Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
S.L.P. 10
Dodoma

Simu: +255 262 963 533
Baruapepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

YALIYOMO

Idhini iii

1.0 Taarifa za Awali 1

1.1 Utangulizi 1

1.2 Muundo wa Muhtasari 1

1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari 2

1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania 2

1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 3

1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 4

1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu 4

1.8 Malengo ya Somo la Lugha ya Alama ya Tanzania 5

1.9 Upimaji na Tathmini 6

1.10 Muda wa Mafunzo 7

1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo 7

2.0 Maudhui ya Muhtasari 8

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo 8

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo 10

Majedwali

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati 6

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Uziwi 8

Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Uziwi 10

Orodha ya Machapisho 26

1.0 TAARIFA ZA AWALI

1.1 Utangulizi

Muhtasari huu wa somo la Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) umeandaliwa kutokana na Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu wa mwaka 2019. Muhtasari huu unalenga kumjengea mwalimu tarajali maarifa, stadi na mwelekeo utakaomwezesha kukabiliana na mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi kiziwi aliyedahiliwa katika elimu ya msingi.

Ili kumsaidia mkufunzi, yametolewa mapendekezo ya mbinu za kufundishia na kujifunzia, zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na upimaji. Mkufunzi anahimizwa kutumia mbinu mbalimbali na zana zinazopatikana kwenye mazingira yanayohusika na upimaji ulioshauriwa kwenye muhtasari huu. Pamoja na mbinu zilizoainishwa kwenye muhtasari huu mkufunzi anaweza kutumia mbinu nyingine tofautitofauti kulingana na mazingira na mahitaji ya mwalimu tarajali na umahiri unaojengwa.

1.2 Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ina taarifa za awali na sehemu ya pili ni maudhui ya muhtasari.

Sehemu ya kwanza inajumuisha utangulizi, muundo wa muhtasari, sababu za kuandaa muhtasari, malengo ya elimu nchini Tanzania, malengo ya jumla ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, madhumuni ya mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, umahiri wa jumla wa mafunzo ya astashahada ya ualimu elimu maalumu, malengo ya somo la Lugha ya Alama ya Tanzania, upimaji na tathmini na muda wa mafunzo. Sehemu ya pili inajumuisha maudhui ya muhtasari wa somo.

1.3 Sababu za Kuandaa Muhtasari

Dira ya elimu na mafunzo inasisitiza kuwapo kwa mwalimu aliye bora kitaaluma na kitaalamu na mwenye mbinu mbalimbali za kujifunzia na kufundishia somo la Lugha ya Alama ya Tanzania ili kukabiliana na changamoto za mahitaji na matarajio ya kielimu kulingana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Mwelekeo wa dira na mpango wa elimu kwa ujumla ni kumwandaa mwalimu mwenye ujuzi na stadi za Lugha ya Alama ya Tanzania katika shule za msingi kwa kuzingatia misingi, kanuni na mielekeo inayopasa. Mwalimu tarajali wa somo la Lugha ya Alama ya Tanzania kwa ajili ya mwanafunzi kiziwi anahitaji kupata ujuzi wa kuweza kuyatumia vema mazingira yake katika kuwezesha mawasiliano na mwanafunzi kiziwi.

1.4 Malengo ya Elimu Nchini Tanzania

Elimu inayotolewa ni ya kurithisha maarifa, stadi na mielekeo bora kutoka kwa vizazi vilivyopita hadi vizazi vya wakati huu na vijavyo. Hivyo, yafuatayo ndiyo malengo makuu ya elimu nchini:

a) kuendeleza na kukuza maendeleo, kuboresha haiba ya wananchi wa Tanzania, rasilimali zao na matumizi bora ya rasilimali hizo katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na ya kitaifa;
b) kukuza tabia ya kuthamini utamaduni, mila na desturi za watanzania;
c) kukuza upatikanaji wa fursa za kusoma, kuandika na kuhesabu na matumizi sahihi ya maarifa na stadi za kijamii, kisayansi, kiufundi, kiteknolojia, kitaalamu na aina nyingine za maarifa na ujuzi, kwa ajili ya maendeleo na kuboresha hali ya mtu na jamii;
d) kukuza na kuendeleza kujiamini, kudadisi, weledi na kuheshimu utu wa mtu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza na kwa maendeleo ya Taifa;
e) kuwezesha na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, kuboresha na kukuza stadi za kiakili, utendaji, uzalishaji na nyingine zinazotakiwa katika kukidhi mabadiliko ya mahitaji kiuchumi;

f) kumwezesha kila raia kuelewa misingi ya katiba ya nchi pamoja na kuthamini haki za binadamu na uraia, wajibu na majukumu yanayoendana nayo;
g) kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi za kujiajiri na kuajiriwa na kuboresha utendaji kazi katika sekta za uzalishaji na huduma;
h) kujenga misingi ya maadili yanayokubalika kitaifa na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na sheria kwa njia ya kujifunza;
i) kuwezesha kuwapo kwa matumizi sahihi, usimamizi na utunzaji wa mazingira; na
j) kujenga tabia na utamaduni wa kuwakubali watu wenye ulemavu na kuwashirikisha kwenye nyanja zote za maisha kwa maendeleo ya Taifa.

1.5 Malengo ya Jumla ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mafunzo ya Ualimu Elimu Maalumu yana malengo yafuatayo:

a) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika nadharia za saikolojia ya elimu, malezi, ushauri na huduma kwa watu wenye ulemavu;
b) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kugundua na kubuni mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia;
c) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika uchambuzi wa mtaala na vifaa vya mtaala;
d) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kumudu stadi kuu za masomo ya lugha, sanaa na maendeleo ya sayansi na teknolojia;
e) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika kufanya upimaji na tathmini ya maendeleo katika elimu;
f) kujenga umahiri kwa mwalimu tarajali katika stadi za uongozi na utawala katika elimu; na
g) kujenga umahiri wa mwalimu tarajali katika kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu.

1.6 Madhumuni ya Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Mwishoni mwa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu ya muda wa miaka miwili, mwalimu tarajali aweze:

a) kutafsiri mtaala wa elimu ya msingi na mihtasari yake katika masomo darasani;
b) kuandaa na kutumia njia shirikishi katika ufundishaji/ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
c) kubuni, kuendeleza na kufaragua zana za ufundishaji na ujifunzaji katika elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
d) kufanya tafiti tatuzi za kielimu ili kuwabaini, kuwaendeleza na kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
e) kurithisha desturi, maadili na tabia zinazokubalika kwa wanafunzi wa shule za msingi;
f) kuchagua, kupanga, kusimamia na kuongoza vipindi darasani katika shule za msingi;
g) kufundisha kwa ufanisi masuala mtambuka; na
h) kutunga na kusahihisha majaribio na mitihani inayoendana na mtaala wa elimu ya msingi kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi katika nyanja zote tatu za kujifunza.

1.7 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu

Umahiri mkuu wa mafunzo ya Astashahada ya Ualimu Elimu Maalumu umejikita katika kumwandaa mwalimu tarajali aweze:

a) kumbaini mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu, kujenga misingi ya kukubalika kwa wenzake, kwa jamii na kumpatia afua stahiki;
b) kutumia mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu;
c) kutumia njia mbalimbali za mawasiliano na teknolojia saidizi kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya mwanafunzi;
d) kutumia mbinu mbalimbali katika kutambua vipaji walivyonavyo wanafunzi wenye mahitaji maalumu na namna ya kuviendeleza;

e) kufanya tafiti tatuzi za kielimu kwa wanafunzi ili kuwabaini na kuwasaidia wale wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi;
f) kutumia misingi na stadi za uongozi katika kuongoza taasisi mbalimbali za elimu;
g) kutumia, kutunza na kukarabati vifaa saidizi vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
h) kutumia sanaa na michezo rekebifu katika kuibua na kuendeleza vipaji mbalimbali vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
i) kutumia misingi ya ufundishaji na ujifunzaji kufundishia masomo ya taaluma;
j) kujenga umahiri wa masomo kwa mwalimu tarajali utakaomwezesha kuelewa masomo vema na hivyo kumfundisha mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu; na
k) kushirikiana na familia za wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika kuwajengea wanafunzi hao kujiamini, tabia ya kujifunza na kukuza vipaji walivyonavyo.

1.8 Malengo ya Lugha ya Alama ya Tanzania kwa Mwalimu Tarajali Fani ya Uziwi

Muhtasari huu wa Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) umeandaliwa ili kumwezesha mkufunzi kumuandaa mwalimu tarajali kufikia malengo yafuatayo:

a) kutumia stadi za lugha kujenga umahiri wa LAT;
b) kutumia umahiri wa LAT kuwasiliana na mwanafunzi kiziwi;
c) kutumia LAT kuwasiliana na jamii ya viziwi inayotumia lugha hiyo;
d) kutumia umahiri wa LAT kuwahamasisha wanafunzi viziwi kujifunza na kuitumia; na
e) kutumia stadi za LAT katika ufundishaji wa masomo mengine.

1.9 Upimaji na Tathmini

Muhtasari huu umependekeza mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini kwa kuzingatia mahitaji ya mwalimu tarajali wakati wa mchakato wa ujifunzaji wa kozi ya ualimu. Upimaji tamati utafanywa na Baraza la Mitihani la Tanzania na utakuwa na alama 50. Upimaji endelevu utafanywa na mkufunzi wakati mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaendelea na utakuwa na alama 50. Upimaji huu unahusisha majaribio, kazimradi, kazi binafsi, mkoba wa kazi, kazi kwa vitendo na mtihani wa mwisho wa muhula. Uzito wa kila aina ya upimaji umeoneshwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali namba 1: Upimaji Endelevu na Upimaji Tamati

Vipengele	**Njia za Upimaji**	**Mwaka**				**Idadi**	**Alama (%)**
		Mwaka wa I		**Mwaka wa II**			
		Muhula wa I	**Muhula wa II**	**Muhula wa I**	**Muhula wa II**		
Taaluma	Majaribio	1	1	1	1	4	10
	Kazimradi	1	-	1	-	2	5
	Kazi binafsi	1	1	1	-	3	5
	Kazi kwa vitendo	1	1	1	-	3	5
	Mkoba wa kazi	1	-	1	-	2	5
	Mtihani wa mwisho wa muhula	1	1	1	-	3	20
Upimaji endelevu							50
Upimaji tamati: Mtihani wa Baraza la Mitihani la Tanzania			Nadharia		1	1	25
			Vitendo		1	1	25
Jumla ya alama za upimaji endelevu na upimaji tamati							**100**

1.10 Muda wa Mafunzo

Muhtasari huu wa somo la Lugha ya Alama ya Tanzania kwa fani ya uziwi umekusudiwa kukamilishwa kwa kipindi cha miaka miwili. Mtazamo wa somo hili ni kumjengea mwalimu tarajali misingi muhimu ya maarifa ya somo la Lugha ya Alama ya Tanzania itakayomwezesha kumfundisha kikamilifu mwanafunzi kiziwi kumudu ujifunzaji katika elimu ya msingi

1.11 Maudhui ya Muhtasari wa Somo

Maudhui ya muhtasari yamepangwa katika jedwali yakihusisha umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali, vigezo vya upimaji, viwango vya utendaji na idadi ya vipindi

1.11.1 Umahiri

Ni uwezo wa kufikiri na kutenda kwa ufanisi

1.11.2 Umahiri Mkuu

Ni uwezo wa kutenda jambo kwa usahihi na ufanisi unaokusudiwa kufikiwa na mwalimu tarajali baada ya kujifunza kwa muda fulani. Hujengwa na umahiri mahususi kadhaa atakaoujenga mwalimu tarajali kwa kutenda shughuli mbalimbali

1.11.3 Umahiri Mahususi

Ni uwezo atakaojengewa mwalimu tarajali katika kutenda shughuli mbalimbali kwa muda maalumu

1.11.4 Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali

Ni vitendo ambavyo mwalimu tarajali anapaswa kuvifanya ili kufikia umahiri mahususi uliokusudiwa

1.11.5 Vigezo vya Upimaji

Ni viwango vya ufanisi wa utendaji wa mwalimu tarajali ili kufikia umahiri mahususi

1.11.6 Viwango vya Utendaji

Ni kiasi cha ufikiwaji wa vigezo vya kila shughuli anayotenda mwalimu tarajali

1.11.7 Idadi ya Vipindi

Idadi ya vipindi ni makadirio ya muda utakaotumika katika kufundishia na kujifunzia kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Somo hili litafundishwa kwa vipindi vinne (4) kwa wiki. Hata hivyo, mapendekezo haya ya idadi ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

2.0 MAUDHUI YA MUHTASARI

2.1 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo

Jedwali namba 2: Umahiri wa Somo la Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Uziwi

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
1.0 Kutumia mazingira ya lugha kueleza hali, historia na maendeleo ya Lugha ya Alama ya Tanzania	1.1 Kueleza dhana ya lugha ya alama 1.2 Kueleza historia na maendeleo ya LAT na lahaja zake 1.3 Kueleza tofauti ya LAT na lugha ya mazungumzo

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
2.0 Kutumia kanuni za LAT kuunda alama za msingi	2.1 Kutambua matumizi ya vijenzi vya LAT 2.2 Kuumba alama za namba na alfabeti kwa kutumia mkono/ mikono 2.3 Kutumia maumbo ya mkono/mikono na mnyumbuko wa mwili kuunda alama 2.4 Kuunda alama za majina ya watu na matendo asilia
3.0 Kutumia kanuni za LAT kuwasiliana kwa ufasaha	3.1 Kutumia viwakilishi na vimilikishi katika mawasiliano 3.2 Kutumia viunganishi, vielezi na vivumishi katika mawasiliano 3.3 Kuunda sentensi sahili na sahihi za LAT 3.4 Kutumia kanuni ya sarufi ya LAT katika kuunda sentensi
4.0 Kutumia stadi za lugha kukuza mawasiliano ya LAT katika taaluma	4.1 Kutumia istilahi/msamiati sahihi wa LAT katika masomo ya Sayansi na Teknolojia na Hisabati 4.2 Kutumia istilahi/msamiati sahihi wa LAT katika masomo ya lugha na Maarifa ya Jamii 4.3 Kutumia istilahi/msamiati sahihi wa LAT katika nyanja za sanaa, michezo, Stadi za Kazi, Uraia na Maadili na Dini 4.4 Kutumia stadi za LAT kujieleza kwa ufasaha

2.2 Maudhui ya Ufundishaji wa Somo

Jedwali namba 3: Maudhui ya Ufundishaji wa Somo la Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) kwa Mwalimu Tarajali wa Fani ya Uziwi

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
1.0 Kutumia mazingira ya lugha kueleza hali, historia na maendeleo ya Lugha ya Alama ya Tanzania	1.1 Kueleza dhana ya lugha ya alama	a) Kueleza dhana ya lugha	Dhana ya lugha imeelezwa.	Anaeleza maana ya lugha.	Anaeleza maana na aina za lugha.	Anaeleza maana, aina na umuhimu wa lugha.	Anaeleza maana, aina, umuhimu wa lugha na kuhusianisha na muktadha.	13
		b) Kueleza dhana ya alama	Dhana ya alama imeelezwa.	Anaeleza maana ya alama.	Anaeleza maana ya alama na ishara katika lugha.	Anaeleza maana na matumizi ya alama na ishara katika lugha.	Anaeleza maana, matumizi ya alama, ishara na tofauti kwa kuhusianisha na muktadha.	
		c) Kueleza dhana ya lugha ya alama	Dhana ya lugha ya alama imeelezwa.	Anaeleza maana ya lugha ya alama.	Anaeleza maana na aina ya lugha ya alama.	Anaeleza maana, aina na umuhimu wa lugha ya alama.	Anaeleza maana, aina, umuhimu wa lugha ya alama na changamoto za lugha ya alama.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
	1.2 Kueleza historia ya maendeleo ya LAT na lahaja zake	a) Kubaini chimbuko la LAT na lahaja zake	Chimbuko la LAT na lahaja zake zimebainishwa.	Anaeleza chimbuko la LAT na lahaja zake na uanzishwaji wa shule za wanafunzi viziwi.	Anaeleza chimbuko la LAT na lahaja zake, uanzishwaji wa shule za wanafunzi viziwi na harakati za CHAVITA	Anaeleza chimbuko la LAT na lahaja, uanzishwaji wa shule za wanafunzi viziwi, harakati za CHAVITA na changamoto zake.	Anaelezea chimbuko la LAT na lahaja zake na uanzishwaji wa shule za wanafunzi viziwi, harakati za CHAVITA, changamoto, na suluhisho zake.	13
		b) Kueleza maendeleo ya LAT	Maendeleo ya LAT yameelezwa.	Anaeleza historia ya kukubalika kwa LAT.	Anaeleza historia ya kukubalika kwa LAT na usanifishaji wake.	Anaeleza historia ya kukubalika kwa LAT, usanifishaji na utunzi wa kamusi.	Anaeleza historia ya kukubalika kwa LAT, usanifishaji, utunzi wa kamusi na matumizi ya LAT kama lugha ya kujifunzia na kufundishia shuleni.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Anaeleza dhana ya utamaduni wa Viziwi	Dhana ya Utamaduni wa viziwi imeelezwa. .	Anaeleza maana ya utamaduni wa viziwi.	Anaeleza maana na umuhimu wa utamaduni wa viziwi.	Anaeleza maana, umuhimu wa utamaduni wa viziwi na matumizi ya lugha ya alama.	Anaeleza maana na umuhimu wa utamaduni wa viziwi, matumizi ya Lugha ya Alama katika mawasiliano na changamoto zake.	
		d) Anaeleza dhana ya jamii ya Viziwi	Dhana ya jamii ya viziwi imeelezwa.	Anaeleza maana ya jamii ya viziwi.	Anaeleza maana na umuhimu wa jamii ya viziwi	Anaeleza maana, umuhimu wa jamii ya viziwi kwa kutoa mifano.	Anaeleza maana na umuhimu wa jamii ya viziwi kwa kutoa mifano na changamoto zake.	
	1.3 Kueleza tofauti ya LAT na lugha ya mazungumzo	a) Kubainisha tofauti kati ya LAT na lugha ya mazungumzo	Tofauti tano kati ya LAT na lugha ya mazungumzo zimebainishwa.	Anabainisha tofauti moja kati ya LAT na lugha ya mazungumzo.	Anabainisha tofauti mbili kati ya LAT na lugha ya mazungumzo.	Anabainisha tofauti tatu kati ya LAT na lugha ya mazungumzo.	Anabainisha tofauti tano na sifa zinazofanana kati ya LAT na lugha ya mazungumzo.	14
		b) Kueleza uhusiano baina ya LAT na Kiswahili	Uhusiano baina ya LAT na Kiswahili umeelezwa.	Anataja alama mbili zenye chimbuko la Kiswahili.	Anataja alama tatu zenye chimbuko la Kiswahili.	Anataja alama nne zenye chimbuko la Kiswahili.	Anataja alama sita zenye chimbuko la Kiswahili na kuzifafanua.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kueleza matumizi ya umbo la mdomo katika LAT	Matumizi ya umbo la mdomo katika LAT yameelezwa.	Anataja umuhimu wa kutumia umbo la mdomo katika kuunda alama kwa kutoa hoja mbili.	Anataja umuhimu wa kutumia umbo la mdomo katika kuunda alama kwa kutoa hoja tatu na kutoa mifano ya alama tano.	Anataja umuhimu wa kutumia umbo la mdomo katika kuunda alama kwa kutoa hoja nne na kutoa mifano ya alama kumi.	Anataja umuhimu wa kutumia umbo la mdomo katika kuunda alama kwa kutoa hoja sita na kutoa mifano ya alama kumi na tano.	
2.0 Kutumia kanuni za LAT kuunda alama za msingi	2.1 Kutambua matumizi ya vijenzi vya LAT	a) Kuelezea maumbo ya mikono katika kuunda alama	Maumbo ya mikono katika kuunda alama yameelezewa.	Anataja maumbo ya mikono katika kuunda alama.	Anataja na kuelezea maumbo ya mikono katika kuunda alama.	Anataja na kuelezea maumbo ya mikono katika kuunda alama kwa mifano.	Anataja na kuelezea maumbo ya mikono katika kuunda alama kwa mifano na kuhusianisha na mazingira.	14
		b) Kufafanua aina za mijongeo ya mikono katika kuunda alama mbalimbali	Aina za mijongeo ya mikono katika kuunda alama zimefafanuliwa.	Anataja aina za mijongeo ya mikono katika kuunda alama.	Anataja na kufafanua aina za mijongeo ya mikono katika kuunda alama.	Anataja na kufafanua aina za mijongeo ya mikono katika kuunda alama na kutoa mifano.	Anataja na kufafanua aina za mijongeo ya mikono katika kuunda alama, kuzihusianisha na kuzitofautisha.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubainisha aina za uelekeo wa mikono katika kuunda alama mbalimbali	Aina za uelekeo wa mikono katika kuunda alama mbalimbali zimebainishwa.	Anataja aina za uelekeo wa mikono katika kuunda alama.	Anataja na kubainisha aina za uelekeo wa mikono katika kuunda alama.	Anataja na kubainisha aina za uelekeo wa mikono katika kuunda alama na kutoa mifano.	Anataja na kubainisha aina za uelekeo wa mikono katika kuunda alama, kuzihusianisha na kuzitofautisha.	
		d) Kubainisha umbo, uelekeo na mjongeo wa mikono katika kuunda alama zinazotumia mikono miwili inayojongea	Umbo, uelekeo na mjongeo wa mikono miwili katika kuunda alama vimebainishwa.	Anataja umbo na uelekeo wa mikono miwili katika kuunda alama.	Anataja na kubainisha umbo, uelekeo na mjongeo wa mikono miwili katika kuunda alama.	Anataja na kubainisha umbo, uelekeo na mjongeo wa mikono miwili katika kuunda alama na kutoa mifano.	Anataja na kuelezea umbo, uelekeo na mjongeo wa mikono miwili katika kuunda alama, anatoa mifano na kuzitofautisha.	
	2.2 Kuumba alama za namba na alfabeti kwa kutumia mkono/ mikono	a) Kubainisha maana, umuhimu na matumizi ya alfabeti na tahajia ya vidole katika LAT	Alama za alfabeti na tahajia ya vidole katika LAT zimeundwa.	Anaelezea maana, umuhimu na matumizi ya alfabeti na tahajia ya vidole.	Anaumba alama kumi na tatu za alfabeti ya LAT (A-M).	Anaumba alama ishirini na sita za alfabeti ya LAT (A-Z).	Anaunda tahajia za maneno na majina mbalimbali kwa kutumia alfabeti ya LAT.	14

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuhesabu namba za kuhesabia kwa kutumia mkono/ mikono	Namba kwa kutumia mkono/mikono zimehesabiwa.	Anahesabu kuanzia 1 hadi 100 kwa kutumia mkono/mikono.	Anahesabu kuanzia namba 1 hadi 1000 kwa kutumia mkono/ mikono.	Anahesabu kuanzia namba 1 hadi 100,000 kwa kutumia mkono/ mikono.	Anahesabu kuanzia namba 1hadi 1,000,000,000 kwa kutumia mkono/ mikono.	
		c) Kuhesabu namba za mpango (mf. -a kwanza, -a pili, -a tatu)	Namba za mpango zimehesabiwa katika LAT.	Anahesabu namba za mpango tatu za kwanza.	Anahesabu namba za mpango tano za kwanza.	Anahesabu namba za mpango kumi za kwanza.	Anahesabu namba za mpango zote pamoja na alama nyingine muhimu za mpango (*mf. mwanzo, mwisho*) na mifano yake.	
	2.3 Kutumia maumbo ya mikono na mnyumbuko wa mwili kuunda alama	a) Kutumia kanuni ya mkono tawala katika kuunda alama	Kanuni ya mkono tawala katika kuunda alama imetumiwa.	Anataja kanuni ya mkono tawala katika kuunda alama.	Anataja na kuelezea kanuni ya mkono tawala katika kuunda alama.	Anataja, kuelezea na kufafanua kanuni ya mkono tawala katika kuunda alama.	Anataja, kuelezea, kufafanua na kutumia kanuni ya mkono tawala katika kuunda alama.	14

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuelezea matumizi ya kanuni ya mikono linganifu katika kuunda alama	Kanuni ya mikono linganifu katika kuunda alama imeelezewa.	Anataja kanuni ya mikono linganifu katika kuunda alama.	Anataja na kuelezea kanuni ya mikono linganifu katika kuunda alama.	Anataja na kuelezea kanuni na umuhimu wa mikono linganifu katika kuunda alama.	Anataja, kuelezea umuhimu na matumizi ya kanuni ya mikono linganifu katika kuunda alama na kutofautisha baina ya jozi za mikono na mijongeo.	
		c) Kuelezea na kutumia viainishi vya LAT	Viainishi vya LAT vimeelezewa na kutumika.	Anataja aina mbili za viainishi vya LAT na kuvielezea.	Anataja aina tatu za viainishi vya LAT na kuvielezea.	Anataja aina nne za viainishi vya LAT na kuvielezea.	Anataja aina za viainishi vya LAT, kuvielezea na kuvitumia.	
		d) Kuunda na kuelezea alama zinazotumia mnyumbuko wa mwili na sura	Alama zinazotumia mnyumbuko wa mwili na sura zimeundwa na kuelezewa.	Anabainisha minyumbuko miwili ya mwili na uso/sura.	Anabainisha minyumbuko mitatu ya mwili na uso/sura na kuelezea.	Anabainisha minyumbuko minne ya mwili na uso/sura na kuelezea.	Anabainisha minyumbuko mitano ya mwili na uso/sura, na kuelezea na kutumia.	
	2.4 Kuunda alama za majina ya watu na matendo asilia	a) Kutumia alama za matendo asilia (*mf. kula, kunywa, kulala*) katika tungo	Alama za matendo asilia zimetumika katika tungo.	Anatumia alama tano za matendo asilia kuunda tungo.	Anatumia alama kumi za matendo asilia kuunda tungo.	Anatumia alama kumi na tano za matendo asilia kuunda tungo.	Anaelezea na anatumia alama ishirini za matendo asilia kuunda tungo.	14

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuunda na kutumia alamajina kwa ajili ya watu	Alamajina kwa ajili ya watu zimeundwa na kutumiwa.	Anaunda na kutumia alamajina kwa watu watatu kwa ajili ya watu.	Anaunda na kutumia alamajina kwa watu watano kwa ajili ya watu.	Anaunda na kutumia alamajina nane kwa ajili ya watu.	Anaunda na kutumia alamajina kwa watu kumi kwa ajili ya watu.	
		c) Kuunda tungo za kusalimiana na kujuliana hali	Tungo za kusalimiana na kujuliana hali zimeundwa.	Anatunga tungo za kusalimiana na wenzake.	Anatunga tungo za kusalimiana na wenzake na majibu yake.	Anatunga tungo za kusalimiana na wenzake, kutoa majibu yake, na kujuliana hali.	Anatunga tungo za kusalimiana, kujuliana hali na wenzake, kutoa majibu yake, na kujadiliana.	
3.0 Kutumia kanuni za LAT kuwasiliana kwa ufasaha	3.1 Kutumia viwakilishi na vimilikishi katika mawasiliano	a) Kuunda tungo zenye viwakilishi vya nafsi (*mf. mimi, wewe, yeye, sisi, hao*)	Tungo zenye viwakilishi vya nafsi zimeundwa.	Anaunda tungo tatu zenye viwakilishi vya nafsi.	Anaunda tungo sita zenye viwakilishi vya nafsi katika kauli ya kutenda.	Anaunda tungo sita zenye viwakilishi vya nafsi katika kauli za kutenda na kutendewa.	Anaunda tungo sita zenye viwakilishi vya nafsi katika kauli za kutenda/ kutendea, kutendewa na kutendeana.	14

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuunda tungo za kutambulishana kwa kutumia viwakilishi vya nafsi (*mf. mimi, wewe, yeye, sisi, hao*)	Tungo za kutambulishana kwa kutumia viwakilishi vya nafsi zimeundwa.	Anaunda tungo za kujitambulisha kwa kutumia viwakilishi vya nafsi.	Anaunda tungo za kujitambulisha na kuwatambulisha wengine kwa kutumia viwakilishi vya nafsi.	Anaunda tungo za kujitambulisha, kuwatambulisha wengine na kutambulishana kwa kutumia viwakilishi vya nafsi.	Anaunda tungo za kujitambulisha, kuwatambulisha wengine, kutambulishana na kutoa maelezo ya ziada kwa kutumia viwakilishi vya nafsi.	
		c) Kuunda tungo zenye vimilikishi (*mf. -angu, -ako, -ake, -etu, -enu, -ao*)	Tungo zenye vimilikishi zimeundwa.	Anaunda tungo zenye vimilikishi vya nafsi (*mf. mbwa wangu, mtoto wako*).	Anaunda tungo zenye vimilikishi vya nafsi na viungo vya mwili (*mf. mkono wako*).	Anaunda tungo zenye vimilikishi vya nafsi vya viungo na vya viumbe wengine (*mf. mkia wa mbwa, mguu wa paka*).	Anaunda tungo zenye vimilikishi vya nafsi za watu, viungo vya mwili na viumbe wengine na kuvifananisha na kuvitofautisha.	
	3.2 Kutumia viunganishi, vielezi na vivumishi katika mawasiliano	a) Kuunda tungo zenye viunganishi (zikilinga nishwa na lugha za maongezi) (*mf. na, lakini, isipokuwa, n.k.*)	Tungo zenye viunganishi kumi na tano zimeundwa kwa LAT.	Anaunda tungo tano zenye viunganishi.	Anaunda tungo nane zenye viunganishi.	Anaunda tungo kumi na mbili zenye viunganishi.	Anaunda tungo kumi na tano zenye viunganishi mbalimbali.	14

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		b) Kuunda tungo zenye muundo wa umoja na wingi (*mf. mmoja, wawili, wengi*)	Tungo kumi na tano za umoja na wingi zimeundwa kwa LAT.	Anaunda tungo tano za umoja na wingi.	Anaunda tungo nane za umoja na wingi.	Anaunda tungo kumi na mbili za umoja na wingi.	Anaunda na kutumia tungo kumi na tano mbalimbali za umoja na wingi.	
		c) Kuunda tungo zenye vielezi (*mf. sana, kabisa, haraka*)	Tungo kumi na tano zenye vielezi zimeundwa kwa LAT.	Anaunda tungo tano zenye vielezi.	Anaunda tungo nane zenye vielezi.	Anaunda tungo kumi na mbili zenye vielezi.	Anaunda tungo kumi na tano mbalimbali zenye vielezi.	
		d) Kuunda tungo zenye vivumishi (*mf. kubwa, dogo, baya, refu*)	Tungo kumi na tano zenye vivumishi zimeundwa kwa LAT.	Anaunda tungo tano zenye vivumishi.	Anaunda tungo nane zenye vivumishi.	Anaunda tungo kumi na mbili zenye vivumishi.	Anaunda tungo kumi na tano mbalimbali zenye vivumishi.	
	3.3 Kuunda sentensi sahili sahihi za LAT (*mf. maswali, majibu, kukanusha*)	a) Kuunda sentensi sahili taarifu	Sentensi sahili taarifu kumi na tano zimeundwa kwa LAT.	Anaunda sentensi sahili taarifu tano.	Anaunda sentensi sahili taarifu nane.	Anaunda sentensi sahili taarifu kumi na mbili.	Anaunda sentensi sahili taarifu kumi na tano za aina mbalimbali.	14
		b) Kuunda sentensi sahili za kuuliza maswali na majibu	Sentensi sahili taarifu kumi na tano zimeundwa kwa LAT.	Anaunda sentensi sahili taarifu tano.	Anaunda sentensi sahili taarifu nane.	Anaunda sentensi sahili taarifu kumi na mbili.	Anaunda sentensi sahili taarifu kumi na tano za aina mbalimbali.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kuunda sentensi sahili kanushi	Sentensi sahili kanushi kumi na tano zimeundwa kwa LAT.	Anaunda sentensi sahili kanushi tano.	Anaunda sentensi sahili kanushi nane.	Anaunda sentensi sahili kanushi kumi na mbili.	Anaunda sentensi sahili kanushi kumi na tano.	
		d) Kuunda sentensi sahili za mshangao	Sentensi sahili za mshangao kumi na tano zimeundwa kwa LAT.	Anaunda sentensi sahili za mshangao tano.	Anaunda sentensi sahili za mshangao nane.	Anaunda sentensi sahili za mshangao kumi na mbili.	Anaunda sentensi sahili za mshangao kumi na tano za aina mbalimbali.	
	3.4 Kutumia kanuni za sarufi ya LAT katika kuunda sentensi	a) Kuunda sentensi kwa kutumia sarufi ya LAT	Sentensi zimeundwa kwa kutumia sarufi ya LAT.	Anaunda sentensi changamano kwa kutumia sarufi ya LAT.	Anaunda sentensi changamano na ambatano kwa kutumia sarufi ya LAT.	Anaunda sentensi changamano, ambatano na shurutia kwa kutumia sarufi ya LAT.	Anaunda sentensi changamano, ambatano na shurutia kwa kutumia sarufi ya LAT na kueleza tofauti zake.	14
		b) Kutofautisha sarufi ya LAT na Kiswahili	Tofauti ya sarufi ya LAT na Kiswahili imeelezwa.	Anaelezea tofauti ya sentensi sahili kwa kutumia LAT na Kiswahili.	Anaelezea tofauti ya sentensi sahili na changamano kwa kutumia LAT na Kiswahili.	Anaelezea tofauti ya sentensi sahili, changamano na ambatano kwa kutumia LAT na Kiswahili.	Anaelezea tofauti ya sentensi sahili, changamano, ambatano na shurutia kwa kutumia LAT na Kiswahili.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubainisha athari za kutumia sarufi ya Kiswahili kwa LAT	Athari za kutumia sarufi ya Kiswahili kwa LAT zimebainishwa.	Anabainisha faida na athari za kutumia sarufi ya Kiswahili kwa LAT.	Anaeleza umuhimu wa kuzingatia sarufi ya LAT na faida za kutumia sarufi ya Kiswahili.	Anaeleza umuhimu wa kuzingatia sarufi ya LAT na athari za kutumia sarufi ya Kiswahili katika LAT.	Anaeleza umuhimu wa kuzingatia sarufi ya LAT na kuchambua athari za kutumia sarufi ya Kiswahili katika LAT na kwa lugha zote mbili.	
4.0 Kutumia stadi za lugha kukuza mawasiliano kwa LAT katika taaluma	4.1 Kutumia istilahi/ msamiati sahihi wa LAT katika masomo ya Sayansi na Teknolojia na Hisabati	a) Kubainisha alama za istilahi/ msamiati katika somo la Sayansi na Teknolojia	Alama hamsini za istilahi/ msamiati katika somo la Sayansi na Teknolojia zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati katika somo la Sayansi na Teknolojia.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati katika somo la Sayansi na Teknolojia.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati katika somo la Sayansi na Teknolojia.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la Sayansi na Teknolojia kwa mifano.	14
		b) Kubainisha alama za msamiati na istilahi katika somo la TEHAMA	Alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la TEHAMA zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati katika somo la TEHAMA.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati katika somo la TEHAMA.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati katika somo la TEHAMA.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la TEHAMA na kuzielezea.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubainisha alama za msamiati na istilahi katika somo la Hisabati	Alama hamsini za istilahi/ msamiati katika somo la Hisabati zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati na matendo katika somo la Hisabati.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati na matendo katika somo la Hisabati.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati na matendo katika somo la Hisabati.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati na matendo katika somo la Hisabati na kuzielezea.	
	4.2 Kutumia istilahi/ msamiati sahihi wa LAT katika masomo ya lugha na Maarifa ya Jamii	a) Kubainisha alama za msamiati na istilahi katika somo la Kiswahili	Alama hamsini za istilahi/ msamiati katika somo la Kiswahili zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati na matendo katika somo la Kiswahili.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati na matendo katika somo la Kiswahili.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati na matendo katika somo la Kiswahili.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati na matendo katika somo la Kiswahili na kuzielezea.	14
		b) Kubainisha alama za msamiati na istilahi katika somo la Kiingereza	Alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la Kiingereza zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati na matendo katika somo la Kiingereza.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati na matendo katika somo la Kiingereza.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati na matendo katika somo la Kiingereza.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati na matendo katika somo la Kiingereza na kuzielezea.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kubainisha alama za msamiati na istilahi katika somo la Maarifa ya Jamii	Alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la Maarifa ya Jamii zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati katika somo la Maarifa ya Jamii.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati katika somo la Maarifa ya Jamii.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati katika somo la Maarifa ya Jamii.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la Maarifa ya Jamii na kuzielezea.	
	4.3 Kutumia istilahi/ msamiati sahihi wa LAT katika nyanja za sanaa, michezo, Stadi za Kazi, Uraia na Maadili na Dini	a) Kubainisha alama za msamiati na istilahi katika nyanja za sanaa na michezo	Alama hamsini za istilahi/msamiati katika nyanja za sanaa na michezo zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati katika nyanja za sanaa na michezo.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati katika nyanja za sanaa na michezo.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati katika nyanja za sanaa na michezo.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati katika nyanja za sanaa na michezo na kuzielezea.	14
		b) Kubainisha alama za msamiati na istilahi katika somo la Stadi za Kazi	Alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la Stadi za Kazi zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati katika somo la Stadi za Kazi.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati katika somo la Stadi za Kazi.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati katika somo la Stadi za Kazi.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la Stadi za Kazi na kuzielezea.	
		c) Kubainisha alama za msamiati na istilahi katika somo la Uraia na Maadili	Alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la Uraia na Maadili zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati katika somo la Uraia na Maadili.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati katika somo la Uraia na Maadili.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati katika somo la Uraia na Maadili.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati katika somo la Uraia na Maadili na kuzielezea.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		d) Kubainisha alama za msamiati na istilahi katika nyanja za dini na imani	Alama hamsini za istilahi/msamiati katika nyanja za dini na imani zimebainishwa.	Anabainisha alama kumi za istilahi/msamiati katika nyanja za dini na imani.	Anabainisha alama ishirini za istilahi/msamiati katika nyanja za dini na imani.	Anabainisha alama thelathini za istilahi/ msamiati katika nyanja za dini na imani.	Anabainisha alama hamsini za istilahi/msamiati katika nyanja za dini na imani na kuzielezea.	
	4.4 Kutumia stadi za LAT kujieleza kwa ufasaha	a) Kusimulia kisa au hadithi kwa LAT	Hadithi moja imesimuliwa kwa LAT.	Anasimulia hadithi moja fupi kwa LAT.	Anasimulia hadithi moja fupi (iliyosomwa darasani) kwa LAT.	Anasikiliza hadithi moja fupi iliyosomwa darasani na kuisimulia upya kwa LAT.	Anaangalia hadithi moja fupi iliyosimuliwa kwa LAT na watu wawili tofauti darasani na kulinganisha.	14
		b) Anafanya igizo la ufundishaji kwa kutumia LAT	Igizo la ufundishaji limefanywa kwa LAT.	Anaigiza kufundisha mada moja ya somo kwa kutumia LAT.	Anaigiza kufundisha mada mbili za somo kwa kutumia LAT.	Anaigiza kufundisha mada mojamoja katika masomo mawili tofauti kwa kutumia LAT.	Anaigiza kufundisha mada mojamoja katika masomo mawili tofauti kwa kutumia LAT na kujibu maswali.	

Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi	Shughuli za Kutendwa na Mwalimu Tarajali	Vigezo vya Upimaji	Upimaji wa Viwango vya Utendaji				Idadi ya Vipindi
				Utendaji Chini ya Wastani	Utendaji wa Wastani	Utendaji Mzuri	Utendaji Mzuri Sana	
		c) Kutumia nyimbo kumfundisha mwanafunzi kiziwi	Nyimbo zimetumika kumfundishia mwanafunzi kiziwi.	Anatoa mfano wa kufundisha kwa kutumia nyimbo mada moja kwa mwanafunzi kiziwi.	Anatoa mifano ya kufundisha mada mbili kwa kutumia nyimbo kwa mwanafunzi kiziwi katika somo moja la elimu ya msingi.	Anatoa mifano ya kufundisha mada tatu kwa kutumia nyimbo kwa mwanafunzi kiziwi katika masomo mawili ya elimu ya msingi.	Anatoa mifano ya kufundisha kwa kutumia nyimbo mada nne katika masomo matatu ya elimu ya msingi.	

Orodha ya Machapisho

Battison, R. (1978). *Lexical borrowing in american sign language.* Silver Spring, United States of America: Linstok Press.

Emmorey, K. (2003). *Perspectives on classifier constructions in sign languages*. New Jersey, London: Lawrence Erlbaum Associates.

Mahwah, N. J. (2003). The presentation of spatial structure in spoken and signed language. In Karen Emmorey (ed.), *Perspectives on Classifier Constructions in Sign Language*. London, United Kingdoms: Lawrence Erlbaum. (pp. 169 - 195).

Muzale, H. R. T. (2004). Kamusi ya lugha ya alama ya Tanzania (Toleo la Pili). *Chama cha Viziwi Tanzania and Department of Languages of Tanzania.* Dar es Salaam, Tanzania: Dar es Salaam University Press.

Muzale, H. R. T. (2009). 'Misingi ya muundo wa lugha ya alama ya Tanzania., *Journal of the Institute of Kiswahili Studies, University of Dar es Salaam, 72*, (2), 1-17.

Muzale, H. R. T. (2009). 'Changamoto za mawasiliano kwa viziwi katika Tanzania., *Journal of the Institute of Kiswahili Studies, University of Dar es Salaam, 72*, (1), 58–95.

Sandler, W. (2012). The phonological organization of sign languages, *Lang Linguist Compass, 6,* (3), 162 - 182.

Valli, C., & Lucas, C. (2001). *Linguistics of american sign language. An Introduction (*3rd ed*.)*. Washington D.C, United states of America: Clerc Books and Callaudet University Press.